N13/2/ABSWA/SP1/SWA/TZ0/XX/T

88132319

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI B – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHÉLI B – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SUAHILI B – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Tuesday 12 November 2013 (afternoon)
Mardi 12 novembre 2013 (après-midi)
Martes 12 de noviembre de 2013 (tarde)

1 h 30 m

---

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for paper 1.
- Answer the questions in the question and answer booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.


© International Baccalaureate Organization 2013

https://xtremepape.rs/

Blank page
Page vierge
Página en blanco



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU A**

# CHUKUA HATUA (TAWI LA OXFAM)

*Linaalika maombi kwa wanaotaka kufanya kazi kwa vipindi vya redio kuendeleza haki jamii*

Oxfam ni shirika la Kimataifa lisilo la Kiserikali na linaloshirikiana na wengine katika kuondoa umasikini nchini Tanzania na katika nchi nyingine zaidi ya 80 duniani. Oxfam Tanzania ilikaribisha maombi ya nia kwa ajili ya zoezi la kutambua na kuwafundisha wasanii kwa ajili ya kuandaa maigizo kwa njia ya redio. Hii ikiwa kama sehemu moja wapo ya vipindi vya redio vya program ya utawala bora ya Chakua Hatua.

Kama jina linavyojieleza, Chukua Hatua ni moja ya eneo la Haki Jamii la Oxfam linalolenga kujenga wanaume na wanawake wanaodai haki zao za kilimo, ufugaji, elimu na huduma zingine za kijamii. Pamoja na kuwezesha mamlaka husika hasa zile zinazoongozwa na wanawake katika kuhakikisha zinashirikisha wananchi katika mchakato mzima wa utoaji maamuzi na sera zinazohusu mustakabali wao hasa katika wilaya za mkoa wa Shinyanga, Geita, Simiyu na wilaya ya Ngorongoro mkoani Arusha. Programu ya redio ya Chukua Hatua imelenga zaidi kwenye Uhamasishaji, Ushawishi wa Kutenda, Majadiliano na Uwajibikaji toka kwa watendaji husika. Maigizo haya ya redio yatelenga katika kufanikisha malengo ya vipindi vya redio vya Chukua Hatua ambavyo vimeshaanzwa kurushwa.

Atakeyefanya kazi hii ni lazima awe na taaluma na uzoefu wa kutosha katika masuala ya utawala bora, ufahamu wa kutosha wa vyombo vya habari na hasa sanaa kwa njia ya redio pamoja uelewa mkubwa wa dhana ya maendeleo vijijini Tanzania na awe na uwezo mkubwa wa kuandika na kuongoza. Tunashauri walio mkoa wa Shinyanga kutuma maombi haya.

Hadidu Rejea za kufanya kazi hii itatolewa kwa wale watakaoleta maombi ya nia.

Kwa wale wanaotaka kuandaa mwongozo huu watume maombi ya nia kwa mujibu wa maelezo hapo juu kwa Kisuma Mapunda kupitia barua pepe kmapunda@oxfam.org.uk. Mwisho wa kupokea maombi ya nia ni Ijumaa tarehe 1 Februari 2013.

*Nipashe* (2013)



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU B**

# MATUMIZI YA SIMU TAMBA MAABADINI

**Kiongozi:** Waumini wenzangu, nimewaita hapa kama viongozi wa maabadi haya. Nataka tushauriane kuhusu tatizo sugu ambalo limetukabili na limenichukiza siku nenda siku rudi.

**Wote:** Tatizo gani hilo, Kiongozi?

**Kiongozi:** Nyote mwafahamu kuwa tunaishi katika ulimwengu unaobadilika kwa kasi sana. Baadhi ya mabadiliko ni mazuri lakini kwa wakati uo huo huwa na madhara fulani.

**Bibi 1:** Unamaanisha nini?

**Kiongozi:** Ehhh! Mojawapo ya nyanja zilizopata mabadiliko makubwa na ya ghafla ni uwanja wa mawasiliano ya simu.

**Mzee 1:** Sasa tuna simu tamba ambazo zimekuja kutuauni sana. Simu hizi ni rahisi na hazina gharama kama simu tuama. Pili, haikulazimu kupoteza wakati nyumbani au ofisini ukisubiri simu. Kifaa unacho mfukoni au mkobani popote uendapo. Unaweza kuipokea au kupiga popote pale. Fauka ya haya, simu tamba zina matumizi mengi muhimu. Kwa mfano, unaweza kutuma au kupokea ujumbe kwa njia ya maandishi.

**Kiongozi:** Mnapozungumzia juu ya simu tamba, hapo ndipo penye kiini cha tatizo letu.

**Wazee:** Simu tamba zimekuwa tatizo vipi?

**Kiongozi:** Samahani sikudhamiria kusema kuwa simu tamba ni tatizo. Simu zenyewe zina manufaa mengi. Hata hivyo, matumizi yake yametokea kuwa tatizo.



https://xtremepape.rs/



**Bibi 1:** Eh! Ni kweli waumini wenzangu kuwa matumizi yamekuwa tatizo?

**Kiongozi:** Ndiyo, matumizi ya simu hizi wakati wa shughuli rasmi kama maombi na mahubiri ni jambo lisilofaa. Kila jambo lina wakati wake. Wakati wa maombi na mahubiri unapaswa kuwa mtulivu na makini, lakini unapojikaza kuhubiri unasikia mlio hapa mara pale. La shani ni kuwa milio hii yote hukirihi sana.

**Mzee 2:** Wenye simu wamekuwa wakitusumbua sana na miondoko yao hii ya tokatoka nje. Usumbufu wao hukatiza utaratibu wa maombi na mahubiri.

**Bibi 1:** Nakubaliana nanyi kuwa pana dharura ya kutafuta suluhu. Tukikosa kufanya hivi, hali itakuwa mbaya.

**Mzee 2:** Naona uamuzi mzuri ni kuwa na utaratibu wa kuwafukuza nje watu ambao wanatumia simu hizi vibaya.

**Kiongozi:** Tukiwafukuza nje, kuna wale ambao hawatarudi tena. Pia ni jambo la kufedhehesha kumfukuza muumini kadamnasi ya wengine.

**Bibi 2:** Basi tuweke vifaa vya kuzuia matumizi ya simu tamba wakati wa maombi na mahubiri.

**Kiongozi:** Njia hiyo nayo ina hatari zake. Kuna watu ambao huwa na vifaa vya mashine moyoni kuwasaidia katika mapigo ya moyo. Tukitumia vifaa unavyosema, tutahatarisha maisha yao.

Francis Waititu *et al.*, *Kiswahili Fasaha* (2005)



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU C**

# MAFURIKO: HOFU SHULE KUTOFUNGULIWA



Hatima ya shule zinazotumiwa kama kambi za kusitiri waliohama makwao kutokana na mafuriko eneo la Nyanza haijulikani shule zinapofunguliwa leo kwa muhula wa pili. Kulingana na Shirika la Msalaba Mwekundu, shule 20 za msingi zimeathirika Siaya, Gucha, Nyatike, Nyando na Nyakach kwani zinatumiwa kama kambi kwa familia 850.

Mkurugenzi wa shughuli za shirika hilo eneo la Magharibi, Bw. Emmanual Owako aliambia Taifa Leo kuwa shirika hilo linajadiliana kwa kina na jamii zinazopakana na shule hizo kuhusu jinsi watoto watakavyoendelea na masomo.

"Tumejumuisha jamii ili kujadili kinachoweza kufanya kwa familia zinazoachwa bila makao, kwani shule nyingi zinamilikiwa kwa ushirikiano na jamii hizo. Tunatazamia pia kuhamisha familia hizo maeneo mengine yaliyo salama," alisema Bw. Owako.

"Shule zilizoathirika na mafuriko huenda zisifunguliwe kama ilivyopangwa. Kuna mpango wa kujumuisha huduma za shule mbalimbali ili wanafunzi wahudumiwe kwa pamoja," alisema.

"Shule zilizofurika na haziwezi kuhudumu zitajumuishwa na zingine kwa muda. Tutatoa msaada unaohitajika kwa shule zinazohitajika kujumuisha zingine."

Alisema shule ambazo zimeharibika zitatumia hema kama madarasa hadi wakati watakapojenga upya madarasa kwani mijengo mingi iliyoathirika haiwezi kutumika. Mkuu wa Elimu katika Kaunti ya Kisumu, Bi. Beatrice Adu, ameagiza maafisa wakuu wa elimu katika wilaya zilizoathirika na mafuriko ili wabaini iwapo zinaweza kufunguliwa.

"Wakuu wa elimu katika wilaya wanahitajika kutoa ripoti kuhusu uwezekano wa kufunguliwa kwa shule zilizo maeneo yaliyoathirika pakubwa na mafuriko. Baada ya kufanya hivyo, hatua itachukuliwa kuhakikisha watoto hawateseki shule zinapofunguliwa kwa muhula wa pili," Bi. Adu alisema.



https://xtremepape.rs/

Alisema shule ambazo hazitaweza kufunguliwa kutokana na maafuriko zitaongezewa muda wa muhula. “Hadi sasa hakuna shule ambayo imeripoti kuwa haitaweza kufunguliwa lakini iwapo hilo litatokea, itabidi tubadilishe ratiba ili kufidia muda ulioongezewa,” aliongezea Bi. Adu.

Katibu wa muungano wa wazazi na walimu, tawi la Nyanza Bw. Jackson Ogweno, alisema serikali inafaa kuingilia kati na kutoa suluhisho la kudumu katika kukabiliana na mafuriko ili kuzuia hali hiyo kuathiri masomo.

“Serikali inahitajika kutafuta ***[ – X – ]*** la kudumu kukabiliana na mafuriko yanayoshuhudiwa nchini. Hii itasitisha **[ – 26 – ]** mbaya kwa masomo katika shule zinazotumiwa kama **[ – 27 – ]**,” alisema Bw. Ogweno. Mafuriko bado yanaendelea kushuhudiwa maeneo mbalimbali Nyanza hadi sasa. Maafisa wa shirika la Msalaba Mwekundu walisema **[ – 28 – ]** lililoathirika zaidi ni Nyatike katika Kaunti ya Migori ambayo wakaazi wanatumia **[ – 29 – ]** kusafiri vijijini huku shule moja ikiwa imefunikwa kabisa na mafuriko.

*Taifa Leo* (2013)



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU D**

# Mtihani si mwisho! Wasio na matokeo mema wasife moyo

Matokeo ya mtihani ya kidato cha nne (KCSE)[1] ya mwaka uliopita, hatimaye yalitangazwa jana lakini baada ya kuchelewa wiki moja na kuzusha wasiwasi tele miongoni mwa wazazi, walimu na wanafunzi. Hii ndiyo mara ya kwanza kwa matokeo ya mitihani kuchelewa na pia kutangazwa mnamo Machi katika miaka 18 tangu mfumo wa elimu wa 8-4-4[2] ulipoanza. Katika miaka iliyopita, matokeo yamekuwa yakitangazwa mwishoni mwa Februari.

Waziri wa Elimu, akitangaza matokeo hayo hakueleza ni kwa nini yamechelewa mwaka huu. Lakini hiyo si hoja hapa! Wanafunzi waliofanya vyema watashangilia huku wenzao, hasa walioanguka watahuzunika. Huzuni zaidi itawapata wanafunzi 1,022 ambao Waziri alisema matokeo yao yameharamishwa kufuatia visa vya udanganyifu.

Mwaka huu idadi ya wanafunzi hao imeteremka ikilinganishwa na wanafunzi 1,365 ambao matokeo yao yaliharamishwa mnamo mwaka 2002. Hakuna huruma kwa wanafunzi kama hao na walimu, ama maafisa wa mitihani ambao huenda waliwasaidia.

Ni matumaini ya wananchi kwamba walimu na maafisa kama hao wataadhibiwa vikali ili wawe funzo kwa wengine. Kila hatua ni lazima ichukuliwe si tu kupunguza, bali pia kukomesha kabisa visa vya udanganyifu katika mitihani ya kitaifa.

Ingawa wanafunzi wengi wamepita na kustahili kujiunga na vyuo vikuu, matumaini yao yatavurugwa na uhaba wa nafasi katika vyuo vikuu vya kitaifa. Hivyo, itawabidi wengine watakaokosa nafasi na vyuo vingine vya kibinafsi ama kwenda ng’ambo kuendelea na masomo.

Wanafunzi watakaoenda ng’ambo watahitaji pesa. Kila mwaka, kulingana na utafiti Wakenya wanatumia sh 16 bilioni kuwasomesha ng’ambo watoto wao. Hizo ni pesa nyingi sana ambazo serikali inapasa kufikiria kupunguza kwa kuhimiza ujenzi zaidi wa vyuo vikuu nchini.

Lakini pia, Wakenya wanapasa kuachana na kasumba ya kupata shahada. Kuna vyuo vingi vinavyotoa mafunzo mengine ya kitaaluma ambayo wanafunzi wanapaswa kuhimizwa kujiunga navyo badala ya kutumia hela nyingi kwenda ng'ambo.

Kwa ujumla, mitihani si mwisho wa maisha na wanafunzi ambao hawatakuwa na bahati kujiunga na vyuo hivyo, bado wanaweza kujaribu bahati yao kwingineko kwani ni haki yao kama tu wananchi wengine kushiriki katika ujenzi wa taifa.

*Taifa Leo* (2004)

[1] KCSE: mtihani wa kidato cha nne nchini Kenya

[2] 8-4-4: mfumo wa elimu wa miaka minane shule ya Msingi, miaka mine shule ya Upili na miaka minne Chuo Kikuu



https://xtremepape.rs/